



255
255

KIBABII UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

2020/2021 ACADEMIC YEAR
THIRD YEAR FIRST SEMESTER

MAIN EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: KIS 401

COURSE TITLE: KISWAHILI POETRY

DATE: 20/07/2021

TIME: 9:00AM-11:00AM

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**

MUDA: Masaa Mawili (2)

Maswali

1. a) Jadili vigezo vyovyote vinne vinavyotumiwa kuainisha mashairi. (alama 8)

b) Fafanua nadharia zozote mbili zinazoeleza chimbuko la ushairi. (alama 4)

c) Dhihirisha kwa kutoa mifano, hoja zozote nne zinazoonyesha kuwa ushairi wa Kiswahili ni mgumu. (alama 8)

c) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
kwamba tunapokuwa na watoto
daima tumulike jamaa zetu wa kiume
kwa kurunzi kali ya uangalifu?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba wapo wazazi wanatuma watoto
Kwenda kutega mitego ya virinda hoteli
Kusudi kuleta changu na nguru nyumbani
Kupigana na kikosi kikali cha njaa?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba baadhi ya wakembe wa kike
Hutiririkwa na machozi na damu
Baada ya wazazi wao halisi wa kiume
Kuwasagasaga kama nyama ya sambusa?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba leo katika baadhi ya nyumba
Wake wanapokuwa katika shughuli za nje
Nyadhifa zao kuu za usiku wa manane
Hutekelezwa kikamilifu na mabinti?

i) Kwa kutoa mifano, bainisha maudhui yoyote manne yaliyoshughulikiwa katika shairi hili. (alama 8)

ii) Eleza bahari zozote mbili za shairi hili. (alama 2)

2. Jadili fani ya mtunzi katika *Utenzi wa Al-Inkishafi*. (alama 20)

3. Fafanua kwa kina taswira ya mwanamke kwa kurejelea *Utenzi wa Jawabu la Mwana Kupona*. (alama 20)

4. Jadili namna mmoja wa watunzi wafuatao walivyoshughulikia suala la uongozi katika bara la Afrika. (alama 20)
- a) *Msimu wa Tisa* -Kithaka wa Mberia (2007)
 - b) *Dhifa*- Euphrase Kezilahabi (2008)
 - c) *Sauti ya Dhiki*- abdilatiff Abdalla (1973)
5. Jadili mgogoro wa ushairi kwa kurejelea hoja zifuatazo: (alama 20)
- i. Arudhi
 - ii. Ugeni
 - iii. Lugha
 - iv. Kijejezi cha ushairi